



# NISHATI

HABARI ZA  
NISHATI

## News **Bulletin**

[www.nishati.go.tz](http://www.nishati.go.tz) [f](#) Wizara ya Nishati [@](#) wizara\_ya\_nishati\_tanzania [@](#) Nishati2017 [W](#) Wizara ya Nishati

Toleo Namba 46

Januari 1 - 31, 2023

### RAIS SAMIA AFUNGA NJIA YA KUCHEPUSHA MAJI NA KUENZA UJAZAJI WA MAJI BWAWA LA JNHPP



**Pata Taarifa uk. 3 hadi 10**

*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan akibonyeza Kitufe kuashiria Hatua ya Kufunga Njia ya Kuchepusha Maji na Kuanza Ujazaji wa Maji kwenye Bwawa la Kuzalisha Umeme (Megawati 2115) la Julius Nyerere JNHPP kwenye Mto Rufiji Mkoani Pwani tarehe 22 Desemba, 2022.*



**LIMEANDALIWA NA KITENGO CHA  
MAWASILIANO SERIKALINI, WIZARA YA NISHATI**

Wasiliana nasi kwa simu namba +255-26-2322018 Nukushi +255-26-2320148 au  
Fika Ofisi ya Mawasiliano, Mji Mpya wa Serikali Mtumba, S.L.P 2494, Dodoma





# BODI YA UHARIRI

**Mwenyekiti**  
Mhandisi Felchesmi Mramba  
Katibu Mkuu

**Makamu Mwenyekiti**  
Kheri Mahimbali

**Mhariri**  
Dorina G. Makaya

**Waandishi**  
Teresia Mhagama  
Zuena Msuya  
Hafsa Omar  
Timotheo Mathayo

**Msanifu Kurasa**  
Lucas Gordon

Wasiliana nasi kwa simu  
namba +255-26-2322018  
Nukushi: +255-26-2320148  
au

Fika Ofisi ya Mawasiliano  
Mitumba Dodoma,  
S.L.P 2494, Dodoma



[www.nishati.go.tz](http://www.nishati.go.tz)

[Wizara ya Nishati](#)

[@Nishati2017](#)

[wizara\\_ya\\_nishati\\_tanzania](#)

[Wizara ya Nishati](#)



## RAIS SAMIA AFUNGA NJIA YA KUCHEPUSHA MAJI NA KUENZA UJAZAJI WA MAJI BWAWA LA JNHPP



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan akisalimiana na Rais Mstaafu wa Awamu ya Pili, Mhe. Ali Hassan Mwinyi alipowasili katika Shughuli ya Kufunga Njia ya Kuchepusha Maji na Kuanza Ujazaji wa Maji kwenye Bwawa la Kuzalisha Umeme la Julius Nyerere (JNHPP) kwenye Mto Rufiji mkoani Pwani*

### ALIOSEMA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, MHE. DKT. SAMIA SULUHU HASSAN

Hili ni tukio muhimu la kihistoria na faraja nchini kwetu katika safari ya kukamilisha mradi wa bwawa la kuzalisha umeme la Julius Nyerere hatua kwa hatua, hii inatoa ujumbe duniani kuwa Tanzania inaweza kutekeleza mambo makubwa ya kuweza kubadilisha taswira ya nchi na ulimwengu pamoja na kuweka alama mpya katika ramani ya dunia.

Mradi huu utatuletea umeme wa uhakika kwa ajili ya maendeleo endelevu na kutimiza ndoto iliyokuwepo tangu tumepata Uhuru, tunawashukuru wote walioshiriki kuleta fikra hii na walioshiriki katika utekelezaji wake.

Nawapongeza sana Wizara ya Nishati, TANESCO, Katibu Mkuu Kiongozi, kampuni, benki, TANAPA, TAWA, TFS, TANROADS, vyombo vya Ulinzi na Usalama, wadau wote wa maendeleo pamoja na wote wanaosaidiana nao kwa kazi nzuri ya usimamizi na utekelezaji inayoendelea kufanywa.

Ujenzi wa Bwawa la Nyerere ni kazi kubwa yenye ubora na viwango vinavyotakiwa, safari ya ujenzi ilianza kipindi cha Mwalimu Nyerere na katika kipindi cha Awamu ya Tano cha Hayati John Pombe Magufuli ujenzi ulianza kutekelezwa, pamoja na mikiki mikiki iliyokuwepo kuhusu suala hili lakini kazi ilianza na kupelekea matunda tunayoyaona hivi leo.



## RAIS SAMIA AFUNGA NJIA YA KUCHEPUSHA MAJI NA KUENZA UJAZAJI WA MAJI BWAWA LA JNHPP



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan akiwapatia tuzo Marais Wastaafu, Mhe. Ali Hassan Mwinyi pamoja na Mhe. Dkt. Jakaya Kikwete kutokana na mchango wao katika utekezaji wa mradi wa umeme wa Julius Nyerere (JNHPP) ambao utazalisha megawati 2115.

### ALIOSEMA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, MHE. DKT. SAMIA SULUHU HASSAN

Naishukuru sana Serikali ya Misri kwa kuwa pamoja nasi, salaam zimfikie Rais wa Misri, Mhe. Abdel Fattah El-Sisi kwa ushirikiano mkubwa anaotupa kwa kuhakikisha mradi huu unatekelezwa ipasavyo.

Wakati napewa jukumu la kuongoza nchi hii mradi huu ulikuwa asilimia 37%, na leo namshukuru Mungu kuona umefikia 78.68%, natoa ahadi kwenu ndugu Watanzania kuwa nitausimamia mradi huu hadi ukamilike kama ulivyopangwa.

Kama tulivyojuzwa hapo awali, hadi sasa kazi imekamilika kwa asilimia 78.68%, kinachoendelea hivi sasa ni kufunga mitambo ya kufua umeme na vifaa vingine kabla hatujaenda kwenye majaribio ya kuiwasha.

Mradi huu ni mojawapo ya miradi mikubwa barani Afrika, Watanzania tuna kila sababu ya kujivunia uwekezaji huu wenye faida nyingi zikiwemo za kuweka akiba kubwa ya maji na kuzalisha umeme hata kama mvua imepungua na kusaidia kudhibiti mafuriko ya mara kwa mara ya mto Rufiji.

Mradi pia utasaidia katika kilimo cha uhakika cha umwagiliaji, utaimarisha na kufungua fursa nyingi za utalii katika eneo la Kusini mwa Tanzania hasa katika Hifadhi ya Taifa ya Nyerere na hivyo kutoa ajira za moja kwa moja na nyinginezo.

Kupitia Bwawa hili, tumejenga daraja kubwa na bora kuiunganisha mikoa ya Kusini, kilichobakia ni barabara ambapo nawaelekeza Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (TANROADS) kuandaa mradi wa ujenzi wa barabara kutoka Chalinze hadi Utete kupitia kwenye daraja hili, lengo ni kwamba watu wanaotoka Mtwara na Lindi kwenda Dodoma, Iringa au Arusha hatakuwa na haja ya kupitia Dar es Salaam hivyo njia hii itafupisha sana safari hizo.



# RAIS SAMIA AFUNGA NJIA YA KUCHEPUSHA MAJI NA KUENZA UJAZAJI WA MAJI BWAWA LA JNHPP



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan akimsikiliza, Waziri wa Nishati Mhe. January Makamba kuhusu Kituo cha Kusafirishia Umeme (Switchyard) katika Mradi wa kuzalisha umeme wa Julius Nyerere (JNHPP) katika Mto Rufiji Mkoani Pwani.

## ALIOSEMA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, MHE. DKT. SAMIA SULUHU HASSAN

Naielekeza Wizara ya Uvuvi na Mifugo kuja na mipango mkakati ya ufugaji wa kisasa wa samaki ili tukuze uchumi wa watu wetu wa maeneo haya.

Naielekeza Wizara ya Kilimo kwa kushirikiana na Wizara ya Aridhi, TAMISEMI na mamlaka nyinginezo mkapime maeneo hayo kwa kuyaweka kwenye mashamba makubwa kwa ajili ya kufanya mnada wa uwazi kwa wawekezaji wa uhakika katika kilimo, pia kwa ajili ya wakulima wadogo wadogo yatakayokuwa na miundombinu ya umwagiliaji.

Manufaa ya bwawa hili katika nyanja zote yatawezekana kama tutatunza mazingira katika vyanzo na mabonde ya mito inayoleta maji hapa bwawani, tutunze mazingira maana huu mradi tumeujenga kwa gharama kubwa na kujinyima vitu vingi muhimu, hivyo tutunze kufa na kupona.

Maji yanayopita hapa ni mengi sana, yanaweza kisaidia mahitaji ya maji safi na salama kwa mkoa wa Dar es Salaam na viunga vyake, namwelekeza Waziri wa Maji kwamba DAWASA iangalie namna ya kuyatumia maji haya na ujenzi wa bwawa hili utoe fursa ya kuanza mipango ya ujenzi wa kituo cha kupokelea maji katika eneo la Mloka ili maji hayo yaanze kutumika Dar es Salaam.

Hakuna mkubwa mbele ya sheria, Wakuu wa Mikoa na Wilaya fanyeni kazi yenu bwawa hili lilindwe ipasavyo. Mto Ruaha Mkuu utachangia maji kwenye bwawa hili kwa 15%, Mto Kilombero utachangia 65%, Mto Luega utachangia 19%, hivyo watu wa maeneo hayo watunze mazingira ili kujaza bwawa la Nyerere.

Wananchi, wafanyabiashara na taasisi zote ambazo zinachepusha maji katika bonde la mto Rufiji waziwe

Siku chache zijazo tunasherehekea Siku Kuu ya Krismasi na Mwaka Mpya, nawatakia Wananchi wote heri nyingi na kuwaomba kuwa waangalifu ili tuwe na furaha.



# RAIS SAMIA AFUNGA NJIA YA KUCHEPUSHA MAJI NA KUENZA UJAZAJI WA MAJI BWAWA LA JNHPP



Wananchi pamoja na viongozi mbalimbali wakishuhudia Shughuli ya Kufunga Njia ya Kuchepusha Maji na Kuanza Ujazaji wa Maji kwenye Bwawa la Kuzalisha Umeme la Julius Nyerere (JNHPP) kwenye Mto Rufiji mkoani Pwani.

## ALIYOSEMA SPIKA WA BUNGE LA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, MHE. DKT. TULIA ACKSON

Leo inatengenezwa historia ya kuondoa tatizo la umeme nchini, hii ni suluhu ya kudumu. Niseme tu Rais Samia umefanya, unafanya na kuzidi, hivyo nakupongeza sana.

Utekelezaji wa mradi huu haugusi tu kwenye eneo la kuleta suluhu ya kudumu kwa upatikanaji wa uhakika wa umeme lakini pia unagusa kwenye sekta nyingine muhimu ya upatikanaji wa uhakika wa maji kwa mikoa iliyopo karibu na bwawa hili.

Kwa wingi wa maji haya, tunaamini tutakuwa na uhakika wa kupata chakula cha kutosha cha kulisha Taifa letu na dunia nzima kwani maji yatawasaidia wakulima kumwagilia mazao yao kwa uhakika.

## ALIYOSEMA WAZIRI WA NISHATI, MHE. JANUARY MAKAMBA

Nakushukuru Rais Samia kwa uongozi wako madhubuti katika nchi yetu kwani ushahidi wa uongozi wako, matokeo ya ustawi wa Watanzania unaonekana, pia amani, utulivu, umoja, upendo na mapatano vinaendelea kushamiri nchini.

Kwa mujibu wa mkataba, pale fedha zinapochelewa kulipwa kwa kila hatua huwa kuna adhabu, hatujawahi kuchelewa hata mara moja kufanya malipo ya mradi huu na hadi leo hii hatudaiwi fedha yoyote.

Rais Samia ulipoingia madarakani mradi huu ulikuwa umefikia 37%, katika kipindi cha miezi 20 ya uongozi wako, mradi huu umefikia 78%, tunakushukuru kwa kuusukuma kwa kasi mradi huu.



# RAIS SAMIA AFUNGA NJIA YA KUCHEPUSHA MAJI NA KUENZA UJAZAJI WA MAJI BWAWA LA JNHPP



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan akizungumza na wananchi wakati wa zoezi la Kufunga Njia ya Kuchepusha Maji na Kuanza Ujazaji wa Maji kwenye Bwawa la Kuzalisha Umeme (Megawati 2115) la Julius Nyerere JNHPP kwenye Mto Rufiji Mkoani Pwani tarehe 22 Desemba, 2022.

## ALIOSEMA WAZIRI WA MAJI, NISHATI NA MADINI - ZANZIBAR, MHE. SHAIBU HASSAN KADUARA

Na sisi ni sehemu ya watu tutakaonufaika na uzalishaji wa umeme huu, hivi karibuni tuliondoa changamoto ya muungano ambapo tumekubaliana kuuziana umeme kwa bei nafuu ya Shilingi 130 kwa Uniti moja.

Tunaendelea kukushukuru na kukupongeza kwa kusimamia kwa dhati muungano wetu, tunawapongeza pia TANESCO kwa ushirikiano mkubwa na Shirika letu la Umeme la ZECO.

## ALIOSEMA MKURUGENZI MTENDAJI WA SHIRIKA LA UMEME TANZANIA (TANESCO), MAHARAGE CHANDE

Njia ya kwanza ya mradi huu ilikuwa ni njia ya kuchepusha maji ya mto, ujenzi wa njia ya mchepusho wa maji umefikia 97.97% na 3.2% iliyobaki kumalizika ni kazi ya kufunga lango kuu ya njia ya mchepusho wa maji itakayofanyika leo.

Njia ya kuchepusha maji ina urefu wa mita 703 na upana wa kipenyo cha mita 12, kwa upande wa ujenzi wa tuta kuu umefikia 89.51% huku 10.5% zilizobaki ni kumalizia mageti ili bwawa linapojaa mageti yafunguliwe maji yaweze kutoka.



# RAIS SAMIA AFUNGA NJIA YA KUCHEPUSHA MAJI NA KUENZA UJAZAJI WA MAJI BWAWA LA JNHPP



Baadhi ya Watumishi wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), wakimsikiliza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan wakati wa zoezi la Kufunga Njia ya Kuchepusha Maji na Kuanza Ujazaji wa Maji kwenye Bwawa la Kuzalisha Umeme (Megawati 2115) la Julius Nyerere JNHPP kwenye Mto Rufiji Mkoani Pwani tarehe 22 Desemba, 2022.

## ALIYOSEMA MKURUGENZI MTENDAJI WA SHIRIKA LA UMEME TANZANIA (TANESCO), MAHARAGE CHANDE

Ukuta una uwezo wa kuhifadhi maji lita bilioni 32, maji haya ni mengi zaidi ya maji yanayopatika ziwa Rukwa yakishajaa katika tuta. Huku maji yanayopita katika njia moja ya mashine ni takriban lita 225,000 kwa sekunde.

Mradi huu unakadiriwa kutumia Shilingi trilioni 6.5 ambazo ni fedha zetu zinazotokana na kodi za Watanzania ambapo mpaka kufikia Novemba, Serikali imemlipa Mkandarasi Shilingi trilioni 4.5 sawa na 70% za mradi.

Usimikaji na ufungaji mitambo kwenye jengo la kufulia umeme umefikia 60.46%, ujenzi wa kituo cha kupokea na kusafirisha umeme umefikia 97.20%.

Hadi kufikia mwezi Novemba, 2022, mradi huu umeajiri watu 12,275 ambapo kati ya walioajiriwa, Watanzania ni 11,164 sawa na 90.97%.

Ujenzi wa njia ya kupitisha umeme umefikia 80%, ujenzi wa daraja litakalounganisha mikoa ya kusini na kaskazini umefikia 96.87% na ujenzi wa nyumba za wafanyakazi umefikia 84.89%.

Mradi huu umejengwa kwa kuzingatia mazingira kama miradi mingine ili usilete athari za mazingira. Ukuta uliojengwa kwenye mradi huu una matundu ambayo yatapitisha maji kidogo ili kuhakikisha viumbe na maisha nyuma ya ukuta yanaendelea.



# RAIS SAMIA AFUNGA NJIA YA KUCHEPUSHA MAJI NA KUENZA UJAZAJI WA MAJI BWAWA LA JNHPP



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan akionyesha jambo Marais wastaafu, Jakaya Kikwete na Alhaj Ally Hassan Mwinyi pamoja na viongozi wengine baada ya kubonyeza Kitufe kuashiria Hatua ya Kufunga Njia ya Kuchepusha Maji na Kuanza Ujazaji wa Maji kwenye Bwawa la Kuzalisha Umeme (Megawati 2115) la Julius Nyerere JNHPP kwenye Mto Rufiji Mkoani Pwani tarehe 22 Desemba, 2022.

## ALIYOSEMA MKUU WA MKOA WA PWANI, MHE. ABUBAKAR KUNENGE

Nishati ni muhimu sana kwa mkoa huu kwani ni mkoa wa uwekezaji na biashara, mkoa wa viwanda na kilimo, yote haya yanahitaji zaidi nishati ya umeme, maji na barabara n.k

Bwawa hili lina fursa nyingi, sisi wakazi wa Pwani tumejipanga kuhakikisha ulinzi na usalama wa eneo hili unakuwa ni kipaumbele chetu pia tutalinda mazingira pamoja na vyanzo vya maji.

## ALIYOSEMA MKUU WA MKOA WA MOROGORO, MHE. FATMA MWASSA

Nawakaribisha wote mlijumuika hapa katika kuweka historia ya nchi yetu. Kipekee, tunakushukuru na kukupongeza Rais, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendeleza kutekeleza kwa kasi kubwa mradi huu mkubwa wa bwawa la Julius Nyerere mpaka kufikia hatua hii ambapo utafunga njia ya mchepusho wa maji ya bwawa hili.

Mradi wa bwawa la Mwalimu Nyerere utakapokamilika, 93% ya umeme unaozalishwa nchini kote utakuwa unazalishwa Morogoro kupitia mabwawa ya Kihansi, Kidatu na JK Nyerere.



## RAIS SAMIA AFUNGA NJIA YA KUCHEPUSHA MAJI NA KUENZA UJAZAJI WA MAJI BWAWA LA JNHPP



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan akimsikiliza, Waziri wa Nishati, Mhe. January Makamba pamoja na Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Maharage Chande kuhusiana na jengo la Mitambo (Power House) kwenye madi wa umeme wa Julius Nyerere (MW 2115) la Julius Nyerere JNHPP katika Mto Rufiji

### ALIOSEMA WAZIRI WA MAMBO YA NJE WA SERIKALI YA MISRI, MHE. SAMEH SHOUKRI

Naipongeza Serikali ya Tanzania kwa jitihada kubwa ambazo imezifanya kwa kuthubutu kuanzisha mradi huu, kwa sasa umefikia 78%, tukio hili la ujazaji wa maji ni hatua kubwa katika kufanikisha mradi huu.

Tanzania imewekeza jumla ya Dola za Marekani bilioni 2.9 kwa ajili ya kuzalisha umeme wa Megawati 2115, Mradi wa Kufua Umeme wa Bwawa la Julius Nyerere utabaki kuwa ni moja ya mradi mkubwa wa kimaendeleo katika bara letu.

**IMEANDALIWA NA IDARA YA HABARI - MAELEZO**



## RAIS SAMIA AFUNGA NJIA YA KUCHEPUSHA MAJI NA KUENZA UJAZAJI WA MAJI BWAWA LA JNHPP



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan akiwa katika picha ya pamoja na viongozi na watumishi wa Wizara ya Nishati, wakati wa zoezi la Kufunga Njia ya Kuchepusha Maji na Kuanza Ujazaji wa Maji kwenye Bwawa la Kuzalisha Umeme (Megawati 2115) la Julius Nyerere JNHPP kwenye Mto Rufiji Mkoani Pwani tarehe 22 Desemba, 2022.



Baadhi ya Watumishi wa Wizara ya Nishati, wakimsikiliza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan wakati wa zoezi la Kufunga Njia ya Kuchepusha Maji na Kuanza Ujazaji wa Maji kwenye Bwawa la Kuzalisha Umeme (Megawati 2115) la Julius Nyerere JNHPP kwenye Mto Rufiji Mkoani Pwani tarehe 22 Desemba, 2022.



## Makamu wa Rais wa Kampuni ya Mafuta na Gesi ya Equinor akutana na Waziri Makamba

**Na Timotheo Mathayo,  
Dar es Salaam.**

**W**aziri wa Nishati, Mhe. January Makamba tarehe 8 Disemba, 2022 amekutana na kufanya kikao na Makamu wa Rais wa Kampuni ya Mafuta na Gesi ya Equinor ya Norway, Bi. Nina Koch jijini

Dodoma ili kuzungumzia maandalizi ya Uwekezaji wa mradi wa kuchakata na kusindika gesi asilia (LNG).

Waziri Makamba amesema anaridhishwa na hatua iliyofikiwa na kusisitiza kuwa anatarajia kuona mradi huu ukitekelezwa kwa wakati kama ilivyopangwa ambapo ili kuhakikisha mradi huo unatekelezwa

kwa ufanisi mkubwa Bi. Koch alisisitiza kuwa Equinor ipo tayari kutoa ushirikiano katika uanzishaji wa Ofisi Maalum ya Mradi wa Kuchakata na Kusindika Gesi asilia (LNG Project Office) ambayo itasimamia na kuratibu shughuli za mradi katika kipindi cha ujenzi na uendeshaji.

Bi. Kochi amesema

“kwa uzoefu wangu miradi kama hii, sio rahisi kukubalika moja kwa moja na pande zote yaani Kampuni na Uongozi wa Nchi. Lakini kwa mradi huu, uongozi wa kisiasa na wananchi wote wa Norway wanauunga mkono”.

Kwa sasa timu za majadiliano za upande wa Serikali ya Tanzania na wawekezaji zipo







## Makamu wa Rais wa Kampuni ya Mafuta na Gesi ya Equinor akutana na Waziri Makamba

katika hatua ya Uandishi (drafting) ya mikataba ya mwisho (final agreements)

Katika ziara yake nchini, Bi. Koch alitembelea eneo utakapojengwa mradi huo wa kuchakata na kusindika gesi asilia (LNG) mkoani Lindi. Bi Koch aliipongeza Serikali kwa kuchagua eneo la mradi karibu na kiwanja cha ndege, jambo ambalo litarahisisha usafiri wa wafanyakazi na

vifaa mbalimbali wakati wa ujenzi na uendeshaji wa mradi.

Pia Bi. Koch alitembelea Chuo cha VETA Lindi ambapo Kampuni zinazotarajiwa kuwekeza katika mradi wa LNG, zimekuwa zikitoa ufadhili wa vifaa vya kujifunzia.

Alimueleza Waziri Makamba kuwa lengo la Kampuni ya Equinor ni kuendelea na kuvifadhili vyo mbalimbali hasa vya mikoa ya Lindi na

Mtwara ili kuwajengea uwezo kwa Watanzania waweze kushiriki kikamilifu katika ujenzi na uendeshaji wa mradi wa huo wenye thamani ya zaidi ya trilioni 70.

Katika kikao hicho Waziri Makamba aliambatana na Kamishna wa Mafuta na Gesi wa Wizara ya Nishati, Bw. Michael Mjinja pamoja na Mha. Charles Sangweni Mkurugenzi Mkuu wa PURA.

Kwa upande wa Equinor, Bi Koch aliongozana na Bw. Nizar Damree, Mkuu wa Kitengo cha Mkondo wa Juu Kimataifa, Bw. Nizar Damree Mkuu wa Kitengo cha Mkondo wa Juu Kimataifa, Bi. Unni Fjær Makamu wa Rais na Mkurugenzi Mkuu wa Equinor Tanzania pamoja na Bi. Genevieve Kasanga, Afisa Mawasiliano Equinor Tanzania.



## **Makamu wa Rais wa Kampuni ya Mafuta na Gesi ya Equinor akutana na Waziri Makamba**



*Waziri wa Nishati Mhe. January Makamba akisalimiana na Rais wa Kampuni ya Mafuta na Gesi ya Equinor ya Norway, Bi. Nina Koch jijini Dodoma walipokutana kuzungumzia maandalizi ya Uwekezaji wa mradi wa kuchakata na kusindika gesi asilia (LNG).*



# TANZANIA, ZAMBIA WAKUTANA KUJADILI USALAMA BOMBA LA MAFUTA

**Na Dorina G. Makaya –  
Dar-es-Salaam.**

**W**aziri wa Nishati, Mhe. January Makamba, tarehe 06 Desemba, 2022, aliongoza ujumbe wa Mawaziri watatu wa Tanzania pamoja na wakuu wa vyombo vya ulinzi na usalama na viongozi waandamizi wa Serikali kukutana na ujumbe wa mawaziri watatu wa Zambia katika mkutano wa kujadili

namna ya kuongeza ulinzi na usalama wa bomba la kusafirishia mafuta la TAZAMA (Tanzania Zambia Mafuta).

Mkutano huo uliofanyika jijini Dar-es-salaam, ni matokeo ya kikao cha Rais wa Tanzania Mhe, Dkt. Samia Suluhu Hassan na Rais wa Zambia Mhe. Hakainde Hichilema ambapo marais hawa walikubaliana kuwa, mawaziri husika wa pande zote mbili wakutane ili kuhakikisha usalama wa bomba

la Mafuta la TAZAMA unazingatiwa kufuatia mabadiliko ya matumizi ya bomba la TAZAMA kutoka kusafirisha mafuta ghafi hapo awali, ili kusafirisha mafuta ya dizeli.

Mawaziri hao wametokeleza maagizo ya wakuu wa nchi hizo mbili ikiwa ni katika kuenzi maono ya Hayati baba wa Taifa Mwl. Julius Kambarage Nyerere na Rais wa kwanza wa Zambia Hayati Kenneth David Kaunda katika

kudumisha mahusiano ya kindugu yenye lengo la kukuza uchumi wa nchi hizo mbili ikiwemo suala la bomba la TAZAMA na kukubaliana taratibu za namna ya kuimarisha ulinzi katika bomba la TAZAMA litakalosafirisha mafuta ya dizeli kutoka nchini kwenda katika taifa hilo jirani.

Akizungumza katika kikao hicho kilichofanyika katika ukumbi wa Hyatt Regency Hotel jijini Dar es Salaam, Mhe. January Makamba ameeleza kuwa



*Waziri wa Nishati Mhe. January Makamba akizungumza na Waandishi wa Habari (hawamo pichani) baada ya kumaliza mkutano wa Tanzania na Zambia wa kujadili usalama wa bomba la mafuta la TAZAMA uliofanyika jijini Dar es Salaam tareh 6 Desemba 2022. Kushoto kwake ni Waziri wa Mambo ya Ndani wa Zambia, Mhe. Jack Mwiimbu.*



# TANZANIA, ZAMBIA WAKUTANA KUJADILI USALAMA BOMBA LA MAFUTA

mara baada ya Serikali ya Zambia kubadilisha matumizi ya bomba hilo kutoka kusafirisha mafuta ghafi ili kusafirisha mafuta ya dizeli, bomba hilo kwa sasa litahitaji ulinzi zaidi ili kulinda usafirishwaji wa mafuta hayo suala lililopelekea umuhimu wa viongozi wa pande zote mbili kukutana na kujadili usalama wa bomba hilo.

“Kama mnavyofahamu, Tanzania na Zambia zina ushirikiano wa muda mrefu ulionzishwa na marais waasisi wa nchi hizi mbili, ambao pia unahusisha bomba la

mafuta la TAZAMA. Huko nyuma bomba la TAZAMA lilikuwa linasafirisha mafuta ghafi. Hata hivyo, miaka kadhaa iliyopita Serikali ya Zambia iliamua kubadilisha matumizi ya bomba hilo ili lisafirishe mafuta ya dizeli”. Alieleza Waziri Makamba.

Alisema, uamuzi huo umepelekea haja ya kuimarisha usalama katika maeneo yote yanayopitiwa na bomba hilo ikihusisha pia wananchi wanaoishi jirani na bomba hilo pamoja na vyombo vya ulinzi na usalama vya nchi zote mbili.

“Hii ni kutokana na thamani ya bidhaa itakayokuwa ikisafirishwa kupitia bomba hilo, kwa kuwa ukishaanza kusafirisha mafuta ya dizeli maana yake usalama wa bomba lenyewe unakuwa ni jambo kubwa la kuzingatiwa.

Hii ni kutokana na kuwa, suala la usalama katika mafuta ghafi lilikuwa si hatari sana kama tunavyokwenda kwenye kusafirisha mafuta ya dizeli. kwa hiyo sasa tukaamua Serikali zetu mbili kufanya uratibu wa usalama wa bomba ”

Alisema Waziri Makamba”

Kwa upande wake Waziri wa Nishati wa Zambia Mh. Peter Chibwe Kapala ameeleza kuwa, awali walikuwa wanasafirisha mafuta ghafi kutoka Tanzania kwenda Zambia ambako yanachakatwa.

Alisema, gharama za uendeshaji zilikuwa kubwa na Serikali yao ilikuwa ikitumia ruzuku kubwa katika uendeshaji.

Waziri huyo wa Nishati wa Zambia alieleza zaidi kuwa, sasa wamefanya mabadiliko ili bomba hilo litumike kusafirisha mafuta ambayo tayari yameshachakatwa ( Dizeli) lakini pia ni wakati wa kufikiria ikiwezekana, waweze kujenga bomba la kusafirisha gesi kutoka Tanzania kwenda Zambia hali itakayosaidia kupunguza ukataji miti hovyoka ajili ya mkaa na kuni na kuwezesha kutunza mazingira.

Naye Waziri wa Ulinzi wa Zambia, Mhe. Ambrose Lufuma aliishukuru Serikali ya Tanzania kwa kuwa mwenyeji wa mkutano huo pamoja na timu ya ufundi kwa kufanya kazi nzuri ndani ya siku mbili walizokaa pamoja



Waziri wa Ulinzi wa Zambia Mhe. Ambrose Lufuma akizungumza na Waandishi wa Habari (hawamo pichani) baada ya kumaliza mkutano wa Tanzania na Zambia wa kujadili usalama wa bomba la mafuta la TAZAMA uliofanyika jijini Dar es Salaam tarehe 6 Desemba 2022. Kushoto kwake ni Waziri wa Mambo ya Ndani wa Zambia, Mhe. Jack Mwiimbu.



# TANZANIA, ZAMBIA WAKUTANA KUJADILI USALAMA BOMBA LA MAFUTA



*Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati Mha. Felchesmi Mramba akimsikiliza kwa makini Katibu Mkuu wa Zambia Mha. Himba Cheelo (kushoto) wakati wa mkutano wa Tanzania na Zambia wa kujadili usalama wa bomba la mafuta la TAZAMA uliofanyika jijini Dar es Salaam tarehe 5 na 6 Desemba 2022.*

ambapo, wameweza kuja na mipango mbalimbali itakayotumika kulinda bomba hilo ikiwemo ufungaji wa kamera za CCTV, matumizi ya drones na kuweka askari kwa ajili ya ulinzi wakati wote.

“Sote tunafahamu kuwa bomba la TAZAMA lilikuwa linabeba mafuta ghafi ambayo yalikuwa hayavutii kama haya ya sasa ambayo yatakuwa yameshachakatwa. Hivyo, tunahitaji

kulilinda bomba hili na ndiyo maana tuko hapa kujaribu kuona jinsi tutakavyolilinda. Tumepokea mawazo mbalimbali na tunaendelea kuzungumza juu ya kuongeza ulinzi, ili kuwezesha kuwepo kwa usalama wa bomba masaa ishirini na nne. Tutaweka drones na kamera za ulinzi (CCTV camera) hii yote ni kilitunza na kulilinda

bomba hili.”Alisema Mhe. Lufuma

Mkutano huo uliotanguliwa na mkutano wa Wataalam wa Nishati wa pande zote mbili, kwa upande wa Tanzania, ulihudhuriwa na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, wakuu wa vyombo vya Ulinzi

na Usalama na viongozi waandamizi wa Serikali ambapo upande wa Zambia walishiriki Waziri wa Ulinzi, Mhe. Ambrose Lufuma, Waziri wa Nishati, Mhe. Peter Chibwe Kapala, Waziri wa Mambo ya Ndani na Usalama wa Nchi, Mhe. Jacob, Jack Mwiimbu, Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati pamoja viongozi waandamizi wa Serikali ya Zambia.



**TANZANIA, ZAMBIA WAKUTANA  
KUJADILI USALAMA BOMBA LA MAFUTA**



*Mawaziri wa Tanzania na Zambia wakifuatilia mada kuhusu usalama wa bomba la mafuta wakati wa mkutano wa Tanzania na Zambia wa kujadili usalama wa bomba la mafuta la TAZAMA uliofanyika jijini Dar es Salaam tarehe 6 Desemba 2022.*



*Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati Mha. Felchesmi Mramba akizungumza wakati wa mkutano wa Tanzania na Zambia wa kujadili usalama wa bomba la mafuta la TAZAMA uliofanyika jijini Dar es Salaam tarehe 5 na 6 Desemba 2022. Kushoto kwake akifuatilia kwa makini ni Katibu Mkuu wa Zambia Mha. Himba Cheelo.*





Viongozi wa Wizara ya Nishati wakimsikiliza Mkurugenzi Mkuu wa REA wakati wa hafla ya kusaini mikataba ya Mradi wa Peri Urban awamu ya tatu ambao utapeleka umeme kwenye maeneo 416 katika mikoa 8 ya Mtwara, Singida, Mbeya, Geita, Tabora, Kagera, Kigoma na Tanga yenye thamani ya shilingi bilioni 76.9 tarehe 19 Desemba, 2022 kwenye Ukumbi wa Mikutano wa Julius Nyerere jijini Dar-es-salaam.

Kushoto kwa Waziri Makamba, ni Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato na kulia kwake ni Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Mha. Felchesmi Mramba akifuatiwa na Naibu Katibu Mkuu Kheri Mahimbali.

Aliye katika Meza ya kuzungumzia, ni Mkurugenzi Mkuu wa REA Mha. Hassan Saidy

## VIJJI VYOTE NCHINI KUFIKIWA NA UMEME KABLA YA MWAKA 2025

**Na Dorina G. Makaya - Dar-es-salaam**

Vijiji vyote nchini vitakuwa vimefikwa na umeme kabla ya mwaka 2025.

Kauli hiyo imetolewa na Waziri wa Nishati Mhe. January Makamba tarehe 19 Desemba, 2022 kwa niaba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,

alipokuwa akizungumza na Wakandarasi kwenye hafla ya kusaini mikataba ya ujenzi wa Mradi wa Peri Urban III kati ya Wakala wa Nishati Vijijini (REA) na wakandarasi iliyofanyika kwenye Ukumbi wa Mikutano wa Julius Nyerere jijini Dar-es-salaam.

Waziri Makamba alisisitiza kuwa hiyo ni ahadi ya uhakika ya Serikali, kwa kuwa

itahakikisha umeme unapelekwa katika maeneo yote ya uzalishaji mali, utoaji huduma za Afya, maji na viwanda vya mazao.

Alisema, mikataba hiyo yenye thamani ya shilingi bilioni 76.9 ni ya kupeleka umeme pembezoni mwa miji katika baadhi ya mikoa, kwa kuwa miji inapanuka na kuna maeneo yasiyo na nishati hiyo.

Aliahidi uongozi wa Wizara yake kujielekeza upya katika miradi ya REA, baada ya kubaini kusuasua kwa utekelezaji wa baadhi ya miradi hiyo ya umeme.

Alisema, katika maeneo mengi watu wamekuwa wakishuhudia wakandarasi wakisimika nguzo za umeme na kuondoka, wengine wakiweka nyaya na



# VIJJI VYOTE NCHINI KUFIKIWA NA UMEME KABLA YA MWAKA 2025



Waziri wa Nishati Mhe. January Makamba akizungumza na wakandarasi wakati wa hafla ya kusaini mikatoba ya Mradi wa Peri Urban awamu ya tatu ambao utapeleka umeme kwenye maeneo 416 katika mikoa 8 ya Mtwara, Singida, Mbeya, Geita, Tabora, Kagera, Kigoma na Tanga yenye thamani ya shilingi bilioni 76.9 tarehe 19 Desemba, 2022 kwenye Ukumbi wa Mikutano wa Julius Nyerere jijini Dar-es-salaam.

kuondoka huku wengine wakipima na kutoweka na ikichukua muda mrefu kukamilika.

Waziri Makamba alisema, Rais ametoa maelekezo mahsusi kwamba vijiji vyote hapa nchini vifikiwe na umeme kwa wakati hivyo kasi ya utekelezaji wa maelekezo ya Rais, ni lazima iongezeke na miradi ikamilike kwa wakati.

Alisema taarifa zilizowasilishwa kwenye Mkutano Mkuu wa

Chama Cha Mapinduzi (CCM) hivi karibuni Dodoma, kati ya mikoa 26 ya Tanzania Bara iliyopata fursa ya kuchangia, 19 ilizungumzia umeme vijijini.

“Hatuwezi kuendelea hivi, lazima tubadilishe utaratibu wa kusimamia miradi hii. Haiwezekani, jambo linasua sua alafu wewe hubadilishi wala hushtuki kuhusu namna ya kulifanya tofauti. kuna mambo mengine tutafanya na mengine

tutaiachia bodi na Menejimenti waende wakakae na kuyatafakari namna bora zaidi ya uharakishaji miradi ya kupeleka umeme vijijini. Alisema Waziri Makamba.

Alisema, miongoni mwa mambo yatakayofanywa na Serikali ni kuajiri waratibu wa Miradi ya REA, vijana 130 katika kila Wilaya watakaoishi kwenye maeneo ya miradi.

Alieleza zaidi kuwa, kila wilaya itakuwa na

mtu mahususi kwa kuwa REA haina watumishi kwenye mikoa na wilaya. Watapewa usafiri wa pikipiki, baiskeli, na bajaji na watatoa taarifa za maendeleo ya miradi wizarani na kwa viongozi wa maeneo ya miradi.

“Hivyo, iwapo mkandarasi atachelewa kuleta nyaya au nguzo tutajua siku hiyo hatutangoja mambo yaharibike.” Alifafanua Waziri Makamba.

Alisema, Wizarataweka mfumo wa



Mkurugenzi Mkuu wa REA Mha. Hassan Saidy akizungumza na Wakandarasi wakati wa hafla ya kusaini mikatoba ya Mradi wa Peri Urban awamu ya tatu ambao utapeleka umeme kwenye maeneo 416 katika mikoa 8 ya Mtwara, Singida, Mbeya, Geita, Tabora, Kagera, Kigoma na Tanga yenye thamani ya shilingi bilioni 76.9 tarehe 19 Desemba, 2022 kwenye Ukumbi wa Mikutano wa Julius Nyerere jijini Dar-es-salaam.





*Viongozi mbalimbali kutoka Wizara ya Nishati na REA wakifuatilia hotuba ya Waziri wa Nishati wakati wa Hafla ya kusaini mikataba ya Mradi wa Peri Urban awamu ya tatu ambao utapeleka umeme kwenye maeneo 416 katika mikoa 8 ya Mtwara, Singida, Mbeya, Geita, Tabora, Kagera, Kigoma na Tanga yenye thamani ya shilingi bilioni 76.9 tarehe 19 Desemba, 2022 kwenye Ukumbi wa Mikutano wa Julius Nyerere jijini Dar-es-salaam.*

## VIJJI VYOTE NCHINI KUFIKIWA NA UMEME KABLA YA MWAKA 2025

mawasiliano kati ya waratibu na Wizara ili Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu wapate taarifa ndani ya siku moja kujua nini kinaendelea kwenye mradi.

Kutokana na hali hiyo, alisema, mkandarasi ambaye mpaka sasa amefikisha asilimia 28 tu ya utekelezaji, hataruhusiwa kusaini mkataba mpya wa REA.

Alifahamisha pia kuwa, Wizara inaanza program ya kupeleka umeme vitongojini kwa

kuwa Serikali imefikia asilimia 75 ya kufikisha umeme vijijini.

“Tunapeleka umeme kwenye visiwa, migodini, kwenye viwanda vidogo vidogo, kwenye maeneo ya uzalishaji wa mashambani, viwanda vidogo vya kusindika mazao, na tunazo fedha mahsusi kwa ajili ya kazi hiyo. Umeme tunaoutaka si wa kuwasha taa, bali ni wa kuhamasisha ukuaji wa uchumi, ujasiriamali vijijini. Ndipo thamani ya umeme itaonekana” alisema Waziri.

Aliitaka Menejimenti ya REA ikatafakari namna ya kufanya mabadiliko kwenye usimamizi wa kazi zake na kuja na kitu kitiwacho REA 2.0 yaani REA mpya.

Pia, amewataka waratibu wa miradi ya REA katika kila mkoa na Wilaya kuweka mfumo wa mawasiliano ya moja kwa moja baina yao na makao Makuu ya Wizara kusimamia utekelezaji.

Wakati huo huo, Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato alisema kulikuwa na

changamoto kwenye utekelezaji wa baadhi ya miradi ya REA hivyo, hatua ya kuwa pamoja na wakandarasi na kuwasimamia itasaidia kuwezesha utekelezaji mzuri.

Aliwataka wakandarasi kukamilisha miradi kwa wakati na kuwa na jukumu la kusimamia Mradi huo wa Peri Urban III ili kutimiza azma ya Serikali ya kuwafikishia wananchi wote umeme.





Wakandarasi wa Kampuni ya DIEYNEM CO LTD Mkurugenzi Mkuu Maulid Ngaiwa wa pili kushoto na Katibu wa Kampuni hiyo Novatus Lyimo, wakishuhudia wakati Mkurugenzi Mkuu REA Mha. Hassan Saïdy akisaini Mkataba na kampuni hiyo katika hafla ya kusaini mikataba ya Mradi wa Peri Urban awamu ya tatu kwa wakandarasi mbalimbali walioshinda zabuni ambao utapeleka umeme kwenye maeneo 416 katika mikoa 8 ya Mtwara, Singida, Mbeya, Geita, Tabora, Kagera, Kigoma na Tanga yenye thamani ya shilingi bilioni 76.9 tarehe 19 Desemba, 2022 kwenye Ukumbi wa Mikutano wa Julius Nyerere jijini Dar-es-salaam.

## MAENEO AMBAYO HAJAFIKIWA NA TANESCO KUNEEMEKA NA MRADI WA PERI URBAN

**Na Dorina G. Makaya – Dar-es-salaam**

**M**aeneo ya pembezoni mwa miji ambayo bado hayajaunganishiwa umeme na TANESCO yatanufaika na Mradi wa Peri Urban III.

Hayo yalielezwa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati Mhandisi Felchesmi Mramba kwenye hafla ya utiaji Saini wa mikataba ya ujenzi wa Mradi wa Peri Urban III kati ya Wakala wa Nishati Vijijini (REA) na wakandarasi iliyofanyika Desemba 19, 2022 Dar-es-Salaam.

Mramba alisema, kwa miaka mingi kuna

maeneo ya pembezoni mwa miji yenye maendeleo mazuri, nyumba nzuri na yenye wateja wenye uwezo wa kutumia umeme, lakini kwa sababu mbalimbali, TANESCO haijayafikia.

Alisema, hiyo si kwa sababu TANESCO haioni haja ya kupeleka umeme maeneo hayo, bali ni kutokana na ukweli kuwa, majukumu yake ni mengi na yanakwenda kwa hatua.

“Mradi huu, unasaidia kufikishia umeme wateja wale ambao kwa kiasi kikubwa wapo tayari kupokea umeme lakini miundombinu ya umeme haijafika maeneo hayo.

Mradi wa Peri Urban

III unaokwenda hatua kwa hatua, naamini ni jibu la kuweza kufikisha umeme katika maeneo hayo.” Alisema Mha. Mramba aliyepata huko

nyuma kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika hilo.

Alisema, nia ya uongozi wa Wizara ni kuona kuwa kazi hii inafanyika kwa kasi



Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati Mha. Felchesmi Mramba wakati wa Hafla ya kusaini mikataba ya ujenzi wa Mradi wa Peri Urban III kati ya Wakala wa Nishati Vijijini (REA) na wakandarasi iliyofanyika tarehe 19 Desemba, 2022 kwenye Ukumbi wa Mikutano wa Julius Nyerere jijini Dar-es-salaam



# MAENEO AMBAYO HAJAFIKIWA NA TANESCO KUNEEMEKA NA MRADI WA PERI URBAN

LA YA UTIAJI SAINI MIKATABA  
KELEZAJI MRADI WA KUPELEK  
EME KATIKA MAENEO YALIYOP  
EZONI MWA MIJAWAMU YA TA



Waziri wa Nishati, Mhe. January Makamba (kulia) akiteta jambo na Naibu Waziri wa Nishati Wakili Stephen Byabato wakati wa Hafla ya kusaini mikataba ya ujenzi wa Mradi wa Peri Urban III kati ya Wakala wa Nishati Vijijini (REA) na wakandarasi iliyofanyika tarehe 19 Desemba, 2022 kwenye Ukumbi wa Mikutano wa Julius Nyerere jijini Dar-es-salaam

kubwa kwa sababu miundombinu ipo na kazi ya wakandarasi ni kufanya mwendelezo wa kuwafikia wateja.

Alisema, ni matarajio ya Wizara kuwa, kazi hiyo itafanyika kwa haraka, lakini pia kwa ubora na umakini mkubwa, ili wateja wapate umeme katika viwango vinavyokubalika.

Aliwataka wakandarasi hao kukamilisha miradi hiyo kwa wakati, kwa ubora na kwa kukidhi matarajio na malengo ya miradi ilipokuwa inanzishwa.

Awali, akizungumza na wakandarasi hao, Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA) Mha. Hassan Saidy, aliwataka wakandarasi kutumia hekima na ushirikishaji wananchi na viongozi wao ili kuepuka

malalamiko yasiyo ya lazima wakati wa utekelezaji wa mradi.

Aliwataka wakandarasi hao kushusha vifaa katika maeneo husika ya mradi ili kuepuka usumbufu wa kuwa na mvutano na wananchi kutokana na wakandarasi kuvishusha maeneo kusiko na mradi na kisha kutaka kuvihamishia eneo la mradi.

Kwa niaba ya wakandarasi waliosaini mikataba hiyo, Mrisho Masoud wa Kampuni ya OK Electrical and Electronics Services LTD, alimhakikishia Waziri wa Nishati, January Makamba, aliyekuwa mgeni rasmi katika hafla hiyo kuwa, watatekeleza miradi hiyo kwa ufanisi huku wakitambua kuwa hana mzaha katika kazi.

Mradi wa Peri Urban awamu ya tatu utapeleka umeme kwenye maeneo 416 katika mikoa 8 ya Mtwara, Singida, Mbeya, Geita, Tabora, Kagera, Kigoma na Tanga.

Pia utahusisha ujenzi wa njia za msongo wa


kati wa umeme zenye urefu wa kilometa 447, njia za msongo mdogo wa umeme za urefu wa kilometa 1020, kufunga transformata 417 na kuunganisha wateja wa awali 22,105 kwa shilingi bilioni 76.9.



Wakandarasi wa Mradi wa Peri Urban awamu ya tatu wakifuatilia kwa makini hotuba ya Waziri wa Nishati, Mhe. January Makamba (Hayumo Pichani) wakati wa hafla ya kusaini mikataba ya Mradi wa Peri Urban awamu ya tatu ambao utapeleka umeme kwenye maeneo 416 katika mikoa 8 ya Mtwara, Singida, Mbeya, Geita, Tabora, Kagera, Kigoma na Tanga yenye thamani ya shilingi bilioni 76.9 tarehe 19 Desemba, 2022 kwenye Ukumbi wa Mikutano wa Julius Nyerere, jijini Dar-es-salaam.



**JARIDA HILI LA MTANDAONI HUTOLEWA NA KITENGO  
CHA MAWASILIANO SERIKALINI, WIZARA YA NISHATI**



**Fika Ofisi ya Mawasiliano,**  
Mji Mpya wa Serikali Mtumba, S.L.P. 2494, Dodoma au  
Wasiliana nasikwa **simu namba:** +255-26-2322018  
**Nukushi:** +255-26-2320148